



MAELFU WAJITOKEZA KUMLAKI MAKAMU WA RAIS TUNDUMA



Mamia ya wananchi wa Tunduma walio jitokeza kwenye mukutano wa hadhara wa makamu wa Raisi Mh. Samia Suluhu Hassan tarehe 23/7/2018

"ITUNZENI MIUNDOMBINU ILI IDUMU"

Makamu wa Raisi wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan azindua kituo cha afya Tunduma tarehe 23/7/2018 alipo fanya ziara yake katika mkoa wa Songwe.

Katika uzinduzi huo Mh. Samia Suluhu Hassan alizungumza na watumishi wa Halmashauri ya mji wa Tunduma walio hudhuria uzinduzi na badee alielekeea kwenye mukutano wa hadhara kuzungumza na wananchi wa mji wa Tunduma.

Mh. Samia Suluhu Hassan ali-pozungumza na watumishi alitoa pongezi zake kwa viongozi, watumishi pamoja na wananchi wote kwa kukamilisha ukarabati wa kituo hicho cha afya. Pia aliwashauri watumishi kupima afya zao kwani ili mtu afanye kazi kwa ufanisi ni lazi-ma awe na afya bora.

"Pineni Afya zenu kwani katika kituo hiki nimeona vifaa vingi na vya kisasa kwahiyko mhakikishe mnakua na afya njema ili kuleta ufanisi kwa Taifa.

"NI HERI UTAWALA BORA USIWEPo LAKINI MAENDELEO YAPATIKANE" – MAKAMU WA RAIS

Hayo yalisemwa na makamu wa Rais Mh. Samia Suluhu Hassan alipo ongea na wananchi wa Mji wa Tunduma katika mukutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya shule ya msingi Tunduma ,tarehe 23/7/2018.

Makamu wa rais alikuja Tunduma kuzindua kituo cha Afya Tunduma kilicho fanyiwa ukarabati mkubwa, na baada ya uzinduzi huo alielekeea viwanja vya shule ya msingi Tunduma kwenye mukutano wa hadhara ambapo aliongea na wananchi wa mji wa Tunduma.

Alisema kua Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inajitahidi kwa kiasi kikubwa kudumisha uta-

wala bora kwani matunda yake yanaoneka dhahiri. Alisema utawala bora unapimwa kwa kuona maendeleo yanayo patikana na sio maneno, maendeleo kama ujenzi na ukarabati wa miundombinu hiyo ni ishara tosha kuwa serikali hii inadumisha utawala bora. Alisema *"kama kufanyika kwa maendeleo haya nilyoyaona ni kutokuwa na utawala bora kama asemavyo Mbunge wa Tunduma, ni heri Halmashauri iendelee na kutokuwa na huo utawala bora lakini maendeleo yapatikane"*

Pia alisema mgogoro wa Madi-

wani uliotoka ulisababishwa na watu kuto kufuata sheria. Alisema kila mtu anatakiwa afanye kazi kwa kufuata sheria. Alisema kuwa Halmashauri hii ya Tunduma inaendeshwa kwa misingi ya sheria, kwahiyko kila mtu anapaswa afuate sheria kwa kila anacho kifanya.

Vilevile aliongeza kuwa wafanya biashara wanapaswa kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa. *"kwa walio kimbia nchi kwa sababu hawataki kulipa kodi wamefanya vyema na wabaki hukohuko kwani wametoa fursa kwa wafan-yabiashara wapya"*.



Makamu wa Raisiwa Jamuhuri ya Muungano Tanzania

Mh. Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuzindua kituo cha afya Tunduma



Makamu wa Rais Mh. Samia Suluhu Hassan katikati akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa mkoa wa Songwe pamoja na wa wilaya ya Mombasa, kwenye uzinduzi wa kituo cha afya Tunduma.